# Matumaini kwa wafanyabiashara baada ya Serikali kuahidi kuboresha mazingira



Rais John Magufuli akizungumza na wafanyabiashara katika mkutano uliofanyika Ikulu hivi karibuni. **Picha na Maktaba**

Alawi Masare, Mwananchi

Wadau katika sekta ya biashara nchini wamekuwa wakipigania kuwapo kwa mageuzi na uboreshaji mazingira ya kufanya biashara.

Viongozi wa vyama vya wafanyabiashara wamekuwa wakishawishi Serikali kuboresha utaratibu wa kisheria na kodi.

Changamoto nyingine ni pamoja na miundombinu kama umeme, usafiri, urasimu, rushwa, gharama kubwa za kufanya biashara na ushindani mdogo.

Hata hivyo, wadau wa sekta binafsi wana matumaini ya mabadiliko baada ya Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imeyafanyia kazi baadhi ya masuala yanayokwamisha biashara kukua.

Hivi karibuni, Rais John Magufuli alikutana na wawakilishi wa wafanyabiashara na kuwaambia azma yake kuhusu sekta binafsi katika kipindi chake cha uongozi.

Tayari wafanyabiashara walijengewa imani na utendaji wa Rais huyo mpya katika kipindi cha takriban mwezi mmoja alichokaa madarakani. Hotuba yake iliwaongezea matumaini, kiasi cha kuamini ukurasa mpya unaweza kufunguliwa kwa sekta binafsi.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Reginald Mengi alielezea kuridhishwa na utendaji wa Rais Magufuli alioonyesha muda mfupi tangu aingie madarakani na kutoa matumaini kwa mipango iliyopo ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili wafanyabiashara.

TPSF ni taasisi mwavuli wa mashirika na kampuni katika sekta binafsi na lengo la msingi ni kutetea sera nzuri na mageuzi muhimu katika kuboresha na kuendeleza mazingira ya biashara na uwekezaji. Hufanya mijadala ya moja kwa moja na Serikali au kupitia Baraza la Biashara la Taifa (TNBC).

Sekta binafsi ilitengeneza ajira zipatazo milioni 1.2 2013 na ilichangia trilioni Sh11.9 kati ya Sh19.8 trilioni zilizotengwa bajeti ya Serikali 2014/15," alisema.



Mgambo wa Manispaa ya Moshi, wakizuia wafanyabiashara wadogo kuendesha shughuli zao barabarani. Usumbufu wa mgambo ni moja ya kero zinazolalamikiwa na wajasiriamaii wadogo katika maeneo mbalimbali nchini. Picha na Maktaba

Mengi aliitaka Serikali mpya kushughulikia ufisadi, uwezeshaji wa kiuchumi, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kama vile mapinduzi ya kilimo.

Katika kushughulikia ufisadi, Mengi alisema sekta binafsi inaridhishwa na mpango wa kujenga mahakama maalumu kwa ajili ya kesi za rushwa, pia alipendekeza kufanya marekebisho ya sheria Namba 11 ya mwaka 2007 ya kuzuia na kupambana na rushwa ili kuipa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mamlaka ya kushtaki.

Kuhusu uwezeshaji wa kiuchumi, alipendekeza haja ya kuandaa sera ya maudhui ya ndani (local content policy) ambayo itawezesha wananchi wa Tanzania kushiriki katika sekta mbalimbali za uchumi.

**Ahadi za Magufuli**

Dk Magufuli aliahidi kwamba Serikali yake itajenga mazingira bora kuwezesha sekta binafsi kufanya kazi vizuri na hivyo kutengeneza ajira zaidi kwa Watanzania.

Alisema Serikali ina mipango ya kuondoa kero za kodi kwa wafanyabiashara wadogo na kuondoa urasimu katika utendaji wake, ili kusaidia wawekezaji wa ndani na nje.

Dk Magufuli alitoa mfano wa kodi 26 tofauti zilizowekwa kwa wakulima wa kahawa wa Kagera, hatua ambayo ilisababisha wakulima hao kusafirisha na kuuza bidhaa zao kinyemela Uganda.

"Nataka tufanye kazi kwa umakini, lakini tuweke mbele masilahi ya taifa kwanza. Serikali iko tayari kuwezesha wawekezaji wa ndani ili kuwekeza zaidi katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na mafuta na gesi na viwanda. Kwa nini hatuna uwekezaji katika viwanda vya kusindika? Inakuwaje muuzaji mkuu wa Tanzanite awe India na Kenya wakati madini haya yanapatikana Tanzania? Tukiwawezesha wawekezaji wa ndani, wageni watakapokuja wataingia ubia," alisema.

Alisema Serikali ingependa kuona wananchi wakiwekeza katika sekta mbalimbali ili kuzalisha ajira zaidi pamoja na kulipa kodi.

"Kama mfanyabiashara yeyote anataka kuwekeza kweli halafu akawa anasumbuliwa na ofisa wa Serikali, nijulisheni. Nina uhakika watu kama hao hawatabaki katika utawala wangu," aliongeza.

**TCCIA yapokea hotuba vizuri**

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) Daniel Machemba anasema kuwa alikuwa na matumaini kuwa baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta binafsi zitashughulikiwa, ingawa nyingine zinaweza kuhitaji muda zaidi.

"Nina matumaini anachokifanya Rais Magufuli ni hatua nzuri kutokana na ukweli kwamba ni kwa manufaa ya sekta binafsi na ya umma na kwa ajili ya ustawi wa Watanzania. Sekta binafsi huwa tunaitaka Serikali kutekeleza mambo fulani lakini hata sisi tunahitaji kuwajibika," anasema.

**Ijue BEST**

Mpango wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (BEST) uliundwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wa maendeleo wanne yaani, Sida, DFID, Danida na Ubalozi wa Uholanzi mwaka 2003/04. Madhumuni ni kuboresha mazingira ya biashara kwa kupitia upya taratibu za kisheria zilizopo.

* Mafanikio ya BEST ni pamoja na kuanzishwa na kuimarisha kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania, kuwa wakala wa pamoja wa uwekezaji na kuboresha uwezo wa sekta binafsi kuishawishi Serikali.

**SAUTI ZA WANANCHI**

**Marick Manyamba:**

**Ili kuwapo mazingira mazuri ya biashara, Selikali inatakiwa iandae kongomano kati ya wanyabiashara wadogo na wakubwa ili kujenga urafiki kati yao kwa lengo la kupunguza kodi ambazo siyo za lazima kwa biashara. Utakuta Serikali inalazimisha kutumia mashine za kielektroniki kwa wafanyabiashara wadogo ambao faida yao haikidhi gharama za mashine hizo.**

**Pius Michael**

**Serikali katika mwaka wa fedha wa 2015/16 ishirikishe wadau wa sekta ya madini, kuunda wakala wa Serikali wa kusimamia masoko na bei na usambazaji ndani na nje. Madini yote yatapigwa muhuri wa Tanzania na ndiyo itakuwa muuzaji mkuu. Wawekezaji watasalimisha madini kwa wakala kwa kuyafanyia tathmini kabla ya kuyauza. Lengo liwe ni kupata kodi na fedha za kigeni Hazina, ili kurudisha thamani ya shilingi yetu na kuinua pato la uchumi wa ndani.**

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA
BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo